

MWONGOZO WA MIPANGO MIJI

VIELELEZO VILIVYOMO

01 KWA NINI NI VIZURI KUPANGA?

Ukurasa 3

02 AINA YA MIPANGILIO YA MIJI

Ukurasa 4

03 AINA YA BARABARA

Ukurasa 5

04 JINSI YA KUCHORA MPANGO WA MAKAZI

Ukurasa 6

KWA NINI NI VIZURI KUPANGA?

Manufaa ya upangaji:

- Kuweka utaribu mzuri wa kuishi kwa pamoja.
- Kutumia vizuri eneo la ardhi lililopo.
- Kutenga maeneo ya wazi kwa kupumzikia, na pia kwa ajili ya ujenzi wa shule, zahanati na kadhalika.
- Kuhakikisha kuwa kila eneo linafikika kwa urahisi, linapata hewa nzuri ya kutosha pamoja na mwanga wa kutosha.
- kupunguza gharama za kupitisha bomba za maji pamoja na bomba za maji machafu/taka.
- kuondoa migongano baina ya wakazi wa eneo hilo.



02


AINA YA MIUNDO YA MIJI

Muundo wa mji ni fursa muhimu na ya kipekee kwa ajili ya upangiliaji wa barabara, maeneo ya kupumzika, vitalu vya nyumba na kadhalika. Inafaa kuchagua aina ya muundo wa mji utakaokidhi mahitaji yenu.

MGONGO

Muundo wa aina hii unakuwa na barabara kuu inayopita katikati ya makazi ya watu na unafaa sana kwenye maeneo yenye vitalu vyembamba. Kuujua muundo huu angalia mfano namba 1.


MGONGO



TOMEA

Kwenye aina hii ya muundo, barabara na vitalu vinakuwa vimezunguka maeneo ya kupumzikia ambayo yako katikati ya makazi ya watu. Jinsi ya Kuujua muundo huu angalia mfano namba 2A.

TOMEA



GRIDI

Aina hii ya muundo ni gridi ya mraba au mstahili. Ni muundo mstahili ulio rahisi ambao unafaa kwa kuweka mandhari mazuri hasa kwenye maeneo ya miteremko/miinuko. Jinsi ya kuutumia muundo huu, angalia mfano namba 2B.


GRIDI



BUMBA/VISHADA

Kwenye aina hii ya muundo, vitalu vnapangwa kuzunguka maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kupumzikia watu. Kuujua muundo huu angalia mfano namba 2C.

BUMBA/VISHADA




03

AINA YA BARABARA

Kumbuka kuwa sio barabara zote zenye upana wenye kufanana. Kuna aina nne za barabara zenye upana tofauti:


ATERI BARABARA

Hii ni barabara yenye kuunganisha eneo lenu na maeneo mengine ya mji; ni barabara kubwa kuliko zote na huwa na njia mbili kwa kila upande. Upana wake ni lazima uwe mita 24.




BARABARA UNGANISHI

Inaunganisha makazi yenu na maeneo mengine yanayowazunguka. Upana wake lazima uwe mita 16.




BARABARA ZA MITAA

Hizi zinaunganisha makazi pamoja na mitaa yenyewe kwa yenyewe. Upana wa barabara hizi lazima uwe mita 10.



NJIA ZA KUPITAA KWA MIGUU

Hizi zinaunganisha maeneo ya kupumzikia au miraba pamoja na nyumba za kuishi watu, na zinatumiwa kwa watembea kwa miguu tu. Upana wao ni lazima uwe mita 4.



Mistari inayogawa barabara zinazopita maeneo ya makazi

JINSI YA KUCHORA MIPANGO YA MAKAZI

Ili kuchora mpango wa makazi/viwanja, kwanza unahitaji kuweka ukubwa wa kitalu cha mtu binafsi unachohitaji kukitengeneza. Maelekezo yafuatayo huzingatia kitalu cha **10x20** (200m²), ambayo inaweza kuongezwa kwa urahisi kuunda kitalu cha 20x20 au 20x30. Kwa ujumla, dhana ya msingi na mbinu inavyoonekana hapa inaweza kuchukuliwa kwa urahisi katika kitalu chenye ukubwa wowote.

MFANO WA 1: VIWANJA VYEMBAMBA

KAMA ENEO NI LEMBAMBA NA REFU, FUATA HATUA HIZI WAKATI WA KUPIMA NA KUCHORA:



1. Chora barabara unganishi kuanzia katikati ya kitalu kifupi kwa eneo, kama inavyoonekana kwenye picha.


2. Chora barabara za mitaa kwa utaratibu wa pembe katikati ya njia kuu na ukingo wa kiwanja, kama inavyoonekana kwenye picha. Upana kati ya ekseli mbili usizidi mita 50. Kama kitalu ni zaidi ya urefu wa mita 300, chora njia za watembea kwa miguu ziwe sambamba na njia kuu inayogawa upande mrefu wa kitalu.

3. Tumia upana wa mita 16 kuchora barabara unganishi (mita 8 kwa kila upande wa mstari wa kati), mita 10 kuchora barabara za mitaa (mita 5 kila upande wa mstari wa kati) na mita 4 kuchora njia za watembea kwa miguu.


4. Chora viwanja vyenye ukubwa unaokidhi mahitaji (mf. 10x20, 20x20, n.k.).

5. Tenga asilimia 8 ya maeneo yote ya viwanja kwa ajili ya maeneo ya kupumzikia, asilimia 5 kwa ajili ya shule na nyumba za starehe, vyote vikiwa karibu na barabara kuu.



MGONGO



Mstari wa katikati wa barabara unganishi



Mstari wa katikati wa barabara za mitaa



MFANO WA 2: ENEO LA ARDHI LENYE UMBO LA KAWAIDA




IKIWA ENEO NI TAMBARARE FUATA HATUA ZIFUATAZO:

A) KAMA MNAHITAJI ENEO KUBWA LA KUPUMZIKIA LIWE KATIKATI YA MAKAZI, FANYENI YAFUATAYO:


TOMEA

1. Chora barabara unganishi ili ziunganishe barabara zinazozunguka maeneo ya makazi. Katikati ya eneo ni pale ambapo barabara hizo zinapopishana.



2. Chora eneo la kupumzikia katikati ya eneo la makazi. Ukubwa wa eneo la kupumzikia ni sawa na ukubwa wa eneo lote la makazi gawanya kwa 40. Kwa mfano, kama eneo lote ni la mraba wa mita 90,000, basi eneo la kati kwa ajili ya kupumzikia litakuwa mita za mraba 2,250.

Mstari wa katikati wa barabara unganishi




Eneo la kupumzikia


Mstari wa katikati wa barabara za mitaa

Chora baadhi ya barabara za mitaa kuanzia katikati ya makazi, na nyingine ziwe sambamba na umbopande za makazi. Upana wa vitalu kati ya barabara sambamba ni 40.

3. Tumia upana wa mita 16 kuchora barabara unganishi (mita 8 kila upande wa mstari wa kati wa barabara) na upana wa mita 10 kuchora barabara za mitaa kuunganisha bumba/shada (mita 5 kwa kila upande wa mstari wa kati wa barabara).



4. Chora viwanja vyenye ukubwa unaokidhi mahitaji (mf. 10x20, 20x20, n.k.).



5. Jumla ya ukubwa wa eneo lote likigawanywa kwa 18 ndilo eneo litakalotumika kwa ajili ya maeneo mengine ya kupumzikia. Vipangilie maeneo yake kiasi kwamba vyote havitakuwa zaidi ya umbali wa mita 300 kutoka vilivyopo vingine. Tenga maeneo mengine karibu na maeneo ya kupumzikia kwa ujenzi wa shule na majengo ya starehe.




B) KAMA MNATAKA MUUNDO RAHISI FANYENI YAFUATAYO:


GRIDI

Mstari wa katikati wa barabara


1. Chora barabara unganishi ili iunganishe barabara zilizopo kwenye eneo/makazi.




2. Chora gridi ambayo itatengeneza mistatili yenye ukubwa wa mita 134 kwa mita 96.




3. Tumia upana wa mita 16 kuchora barabara unganishi (mita 8 kila upande wa mstari wa kati) na upana wa mita 10 kuchora barabara za mitaa (mita 5 kila upande wa mstari wa kati).



4. Kwa kila kitalu chora viwanja vyenye ukubwa unaokidhi mahitaji (mf. 10x20, 20x20, n.k.).




5. Tenga maeneo kwa ajili ya kupumzikia, ujenzi wa shule na jengo la starehe, yote yakiwa karibu na barabara/njia kuu.




6. Asilimia 8 ya ukubwa wa eneo lote litengwe kwa ajili ya meneo ya kupumzikia. Asilimia 5 kwa ajili ya maeneo ya shule, na jengo la starehe. Viwanja vyote visiwe mbali ya mita 300 kutoka kwenye maeneo ya kupumzikia.

Kila kiwanja cha kawaida kinapitiwa na barabara (4m)


Ukubwa wa kitalu: 200 m² (10x20)




Ukubwa wa kitalu : 400 m² (20x20)



Ukubwa wa kitalu: 150 m² (10x15)




Ukubwa wa kitalu: 120 m² (10x12, 8x15)



C) KAMA MNAPENDA WAKAZI WAWA NA FURSA YA KUKUTANA MARA KWA MARA, FANYENI YA FUATAYO:


BUMBA/ VISHADA

1. Choreni barabara unganishi ili iweze kukutana na barabara zingine kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kupumzikia.




2. Gawa viwanja kwa utaratibu wa bumba/vishada. Kila kishada kiwe na ukubwa wa mita za mraba 15000. Kwa mfano, kama eneo lote lina ukubwa wa mita za mraba 90,000, basi mtakuwa na vishada 6.

Mstari wa katikati wa barabara unganishi




3. Chora eneo la kupumzikia katikati ya kila kishada; eneo hilo lisipungue ukubwa wa mita za mraba 1200.




Mstari wa katikati wa barabara za mitaa


4. Tumia upana wa mita 16 kuchora barabara unganishi (mita 8 kila upande wa mstari wa kati wa barabara), upana wa mita 10 kuchora barabara za mitaa kuunganizha na barabara kuu na maeneo ya kupumzikia (mita 5 kila upande wa mstari wa kati wa barabara) na upana wa mita 4 kwa ajili ya njia ya watembea kwa miguu, ambazo pia zitaunganisha maeneo yote ya kupumzikia.




5. Tenga maeneo yenye ukubwa unaokidhi mahitaji (mf. 10x20, 20x20, n.k.). Kisha kwenye kila kishada, tenga maeneo ya ujenzi wa shule na jengo la starehe.




Ukubwa wa kitalu: 200 m² (10x20)



Ukubwa wa kitalu: 400 m² (16x25)



Ukubwa wa kitalu: 150 m² (10x15)



Ukubwa wa kitalu: 120 m² (8x15)

